Benki ya Dunia ni Nini

Mwaka 2002 Benki ya Dunia ilipeana bilioni $19.5 kwa nchi zinazoendelea na ilishughulika katika zaidi ya inchi 100 zinazoendeea ikiwa inajumuisha fedha na/ama ujuzi wa kiufundi ili kuziwezesha kupunguza umasikini.

Tunaishi katika ulimwengu wenye utajiri mwingi sana jinsi kuwa pato la dunia ni zaidi ya trilioni $31 kwa mwaka. Katika ulimwengu huu, mtu wa kawaida katika baadhi ya nchi ana pato la zaidi ya $40,000 kwa mwaka. Lakini katika ulimwengu huuhuu, watu bilioni 2.8—zaidi ya nusu ya watu katika nchi zinazoendelea—wanaishi na pato la chini ya $700 kwa mwaka. Kati ya hawa, bilioni 1.2 wana pato la chini ya $1 kwa siku.

Kwa sababu hii, watoto 33,000 hufa *kila siku* katika nchi zinazoendelea. Katika nchi hizi, kwa kila dakika moja, hufa zaidi ya mwanamke mmoja wakati anajifungua. Umasikini unasababisha watoto zaidi ya milioni 100 wasiweze kwenda shule, wengi wao wakiwa wasichana.

Kazi ya kupunguza kiasi hichi cha umasikini, wakati watu waendelea kuongezeka—kwa kiasi cha watu bilioni 3 kwa miaka 50 inayokuja—ni kikubwa.

Benki ya Dunia inafanya kazi kupunguza tofauti hii na igeuze rasilimali za nchi tajiri kuwa namna ya kukuza nchi masikini. Ikiwa mojawapo ya chanzo kikubwa zaidi cha misaada ya maendeleo ulimwenguni, Benki ya Dunia inasaidia juhudi za nchi masikini kujenga mashule na vituo vya afya, kuhakikisha kuweko kwa maji na umeme, vita dhidi ya magonjwa, na kuhifadhi mazingira.

Siyo benki bali ni shirika maalum. Benki ya Dunia siyo “benki” kwa namna neno hili linalofahamika bali ni mojawapo ya mashirika maalum ya Umoja wa Mataifa, na inajumuisha nchi wanachama 184. Nchi hizi zina jukumu la pamoja la namna shirika linavyopata pesa, na pia namna pesa hizi zinavyotumika. Pamoja na jumuiya nyengine ya maendeleo, Benki ya Dunia inatilia mkazo kufikiwa malengo ya Millennium Development Goals [Malengo ya Ulimwengu ya Maendeleo], yaliyokubaliwa na wanachama wa UN [Umoja wa Mataifa] mwaka wa 2000 na yenye lengo la kuupunguza umasikini kabisa.

"World Bank" [Benki ya Dunia] ndilo jina linalotumika kwa sasa kwa International Bank for Reconstruction and Development (IBRD) [Benki ya Dunia ya Urekebishaji na Maendeleo] na International Development Association (IDA) [Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo]. Pamoja, mashirika haya hupeana mikopo kwa riba ya kiwango cha chini, mikopo isiyokuwa ya riba, pamoja na karadha kwa nchi zinazoendelea.

Wataalamu wa maendeleo 10,000 kutoka karibu kila nchi ulimwenguni wanafanya kazi katika makao makuu ya Benki ya Dunia, Washington DC ama katika ofisi zake 109 za nchi.

Bilioni $8.1 za misaada. Kwa kawaida, nchi zenye pato la chini ulimwenguni huwa haziwezi kukopesha pesa katika soko za ulimwengu ama zinaweza kuipata kwa kiasi kikubwa cha riba. Mabali na michango na mikopo kutoka nchi zilizoendelea, nchi hizi hupokea karadha, mikopo isiyokuwa ya riba, pamoja na usaidizi wa kiufundi kutoka kwa Benki ya Dunia ili kuziwezesha kupeana huduma muhimu. Kuhusu mikopo, nchi zina mda wa miaka 35-40 kuyalipa na huwa mda wa miaka 10 kabla kuanza malipo.

> **Katika mwaka wa fedha 2002 IDA ilipeana billioni $8.1 kudhaminia miradi 133 katika nchi 62 zenye mapato ya chini.**

Mikopo isiyokuwa ya riba na udhamini hutoka kwa IDA, chanzo kikubwa zaidi ulimwenguni cha usaidizi wa dharura. Nchi 40 tajiri hupeana fedha za mpango huu kwa kuchangia kila miaka minne. Hazina iliongezwa hivi karibuni mwaka 2002, na karibu ya bilioni $9 kutoka kwa wafadhili na nyengine bilioni $6.6 kutoka kwenye rasilimali za Benki. Wakati huo, wafadhili walikubali kuongeza matumizi ya karadha za IDA grants—

kufikia asilimia 21 ya rasilimali—ili kushughulikia shida maalum, kama janga la HIV/UKIMWI, linalo kumba nchi masikini na zenye athari zaidi ulimwenguni.

Karadha za IDA ni robo ya usaidizi wa kifedha wa Benki. Mbali na fedha za IDA, kiasi kidogo mno cha pato la Benki linatoka kwa nchi wanachama wake.

Bilioni $11.5 za mikopo. Nchi zinazoendelea zenye pato kubwa—baadhi ya hizi zinaweza kupata mikopo kutoka kwa mashirika ya kifedha, lakini kwa kawaida huwa na riba ya juu sana—hupata mikopo kutoka kwa IBRD.

Nchi zinazopata mikopo kutoka kwa IBRD zina mda mrefu zaidi wa kuilipa ikilinganishwa na mikopo ya mabenki ya kibiashara—miaka 15 hadi 20 ikiwa na mda wa miaka mitatu hadi mitano ya kwanza bila malipo ya kiasi cha awali kuanza. Serikali zinazoendelea huomba pesa kwa miradi hususa, ikiwemo: juhudi za kupunguza umasikini, kupeana huduma ya kijamii, uhifadhi wa mazingira, na kutilia mkazo kukua kwa uchumi ambako kutaimarisha hali ya maisha. Katika mwaka wa 2002 IBRD ilipeana mikopo ya kufikia bilioni $11.5 kwa kusaidia miradi 96 katika nchi 40.

Kuchanga Pesa. IBRD huchanga karibu pesa zake zote katika masoko ya fedha ulimwenguni—billion $23 kwa mwaka wa fedha wa 2002. Ikitumia daraja ya mikopo ya AAA, hutoa bondi kuchangia pesa na halafu hupeana kiwangu cha chini cha riba kwa wateja wake.

World Bank Group [Mshikano wa Benki ya Dunia]. Mbali na IBRD na IDA, mashirika mengine matatu yanajumuishwa katika World Bank Group [Mshiko wa Benki ya Dunia]. International Finance Corporation (IFC) [Muungano wa Kimataifa wa Fedha] hutilia nguvu uwekezaji katika sekta ya kibinafsi kwa kusaidia sekta na nchi zenye athari kubwa. Multilateral Investment Guarantee Agency (MIGA) [Shirika la Uthibiti wa Uwekezaji] hupeana hakikisho dhidi ya athari za kisiasa kwa wawekezaji na watoa mikopo katika nchi zinazoendelea, na International Centre for Settlement of Investment Disputes (ICSID) [Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Mizozo ya Uwekezaji] hutatua migogoro kati ya wawekezaji wa kigeni na nchi wanamofanya uwekezaji.

Wema Ulimwenguni. Katika miaka michache iliyopita, Benki ya Dunia imepeana rasilimali kwa shughuli zenye uzito katika ulimwengu. Moja yake ni upunguzaji wa madeni, na kulingana na Heavily Indebted Poor Countries (HIPC) Initiative [Hatua ya Nchi Zenye Madeni Makubwa], nchi masikini 26 zimepata kupunguziwa madeni ambako kumeziwezesha nchi hizi kuokoa bilioni $41 baada ya mda. Pesa zinazookolewa na nchi hizi kwa kulipa madeni zitatumiwa kwa ujenzi wa nyumba, elimu, afya na miradi ya kushughulikia masikini.

Benki ya Dunia, pamoja na nchi 189 na mashirika mbalimbali imejitolea kuwa na ushirika wa kukabiliana na umasikini. Malengo ya Uulimwengu ya Maendeleo yanaeleza malengo hususa ya kujisajili shuleni, vifo vya watoto wadogo, afya ya wanawake waja wazito, magonjwa, na kuhakikisha kuweko kwa maji-malengo yanayotakiwa kupatikana kufikia mwaka 2015.

Kati ya ushirikiano mwengine ulimwenguni, Benki ya Dunia imeweka kusaidia juhudi za kukabiliana na HIV/UKIMWI kuwa kitu cha muhimu zaidi. Benki ni mdhamini mkubwa zaidi tena wa mda mrefu zaidi wa HIV/AIDS programs [Miradi ya HIV/UKIMWI]. Mchango wa sasa wa Benki kwa HIV/UKIMWI ni wa zaidi ya bilioni $1.3, nusu ya kiwango hichi kikiwa ni cha Afrika Kusini mwa-Sahara.

Aina ya shughuli. Kwa sasa, Benki inashughulikia miradi zaidi ya 1,800 na ni kama ambayo miradi hii iko katika sekta za aina zote na katika kila nchi inayoendelea. Miradi mbalimbali ni kama ile ya: mikopo midogo ya Bosnia Herzegovina na juhudi za kufahamisha jamii kuhusu UKIMWI Guinea, kuchangia elimu ya watoto wa kike Bangladesh na kushughulikia kazi za afya huko Mexico, kusaidia ujenzi wa Timor ya Mashariki ilipopata uhuru, ama kusaidia India kurekebisha Gujarat baada ya mtetemeko wa ardhi uliokuwa muharibifu mno.

Mbali na jinsi ya miradi kadhaa, Nchi na Miradi sehemu za kurasa za mtandao huu zina maelezo kuhuhsu shughuli za Benki.

Vishiko vihusishi
Ripoti ya Mwaka
Taarifa ya Maswala- maoni kuhusu maswala

Nchi Wanachama
Mambo Kumi Ambayo Hukujuwa…